JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na. FB.111/192/01/56** **10 Julai, 2026**

**Kwa Taasisi Nunuzi Zote,**

**Yah: <u>TAARIFA YA KUONGEZWA KWA MUDA WA USAJILI KWA AJILI YA KUSHIRIKI KONGAMANO LA KUMI LA UNUNUZI WA UMMA LA MWAKA 2026</u>**

1. Tafadhali rejeeni barua ya Mamlaka yenye Kumb. Na. FB.111/192/01/38 ya tarehe 30 Aprili 2026 kuhusu mwaliko wa kushiriki Kongamano la Kumi la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2026.

2. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuwajulisha kuwa muda wa usajili kwa ajili ya kushiriki Kongamano hilo umeongezwa hadi tarehe 26 Julai 2026. **Pamoja na nyongeza hiyo, tarehe za kufanyika kwa Kongamano hazijabadilika.** Kongamano litafanyika kuanzia tarehe **29 hadi 31 Julai 2026** katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), Jijini Arusha.

3. Wanaopaswa kushiriki Kongamano hili ni Maafisa Masuuli, Wajumbe wa bodi za zabuni, Maafisa ununuzi, Wanasheria, Wakaguzi wa ndani, Wahandisi, Watumishi kutoka Idara tumizi, Wazabuni, na wengineo. Usajili unafanyika kupitia Mfumo wa Mafunzo wa PPRA kwa anuani https://tsms.ppra.go.tz/ . Ada ya ushiriki ni shilingi 600,000 kwa kila mshiriki.

4. Kwa taarifa au ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na **Bw. Fikiri Ngakonda,** kupitia namba ***0714 928 154 barua pepe:*** *fikiri.ngakonda@ppra.go.tz*.

5. Asanteni kwa ushirikiano wenu.

*Mha.* A. J. Suluo
*Kny:* **MKURUGENZI MKUU**



Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma